# CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO
# (NYUMBA SACCOS LTD)
# NAMBA YA USAJILI DSR 1904

# MWONGOZO WA MATUMIZI YA MFUKO WA TAHADHARI


**EMAIL: info@nyumbasaccos.co.tz**
**S.L.P 45674, DAR ES SALAAM**
**SIMU: 022 2850129**
**: 0746 436049**



**TOLEO LA II: 2023**

# YALIYOMO

**SURA YA KWANZA .......................................................................................... 1**

**1.0 UTANGULIZI ............................................................................................ 1**

1.1 Historia ya Chama ..........................................................................................1

1.2 MFUKO ............................................................................................................1

1.3 MADHUMUNI YA MFUKO ..............................................................................1

1.4 UMILIKI WA MFUKO .......................................................................................2

1.5 UCHANGIAJI WA MFUKO HUU .....................................................................2

1.6 HIFADHI YA FEDHA ZA MFUKO ...................................................................2

1.7 MAFAO YATOKANAYO NA MFUKO HUU.......................................................2

1.8 UTARATIBU WA KUWASILISHA MAOMBI PAMOJA NA NYARAKA ZA KUAMBATANISHA ...........................................................................................3

1.9 MAJUKUMU YA BODI JUU YA MFUKO ..........................................................4

1.10 UHUISHAJI NA UIDHINISHAJI WA MWONGOZO WA MFUKO.........................4

1.10.1 Uhuishaji wa Mwongozo..................................................................................4

1.10.2 Uidhinishwaji wa Mwongozo ...........................................................................4

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Historia ya Chama

NYUMBA SACCOS LTD ni Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo kilichosajiriwa kwa nambari ya usajili 1904 mnamo tarehe 18 mwezi Juni 1969 kikiwa na Wanachama 103 wote wakiwa wafanyakazi wa Shirika la Nyumba la Taifa. Wakati huo Chama kilijulikana kwa jina la NYUSA, na baadae kubadilishwa jina na kuwa Nyumba Savings and Credit Co-operative Society Ltd (NYUMBA SACCOS LTD) kutokana na mahitaji ya Sheria mpya ya Vyama vya Ushirika Na. 20 ya mwaka 2003 wakati huo na Kanuni zake za mwaka 2004 kama ilivyofutwa na kuendelea kutambulika kwa yote yaliofanywa chini ya Sheria hiyo na Kifungu cha 144(2) cha Sheria ya Vyama vya Ushirika nambari 6 ya mwaka 2013.

NYUMBA SACCOS LTD ilianzishwa baada ya kuona kuwa Wafanyakazi wanapata changamoto kubwa katika kupata fedha za kuanzisha/ kutekeleza shughuli zao mbalimbali ziwe za kiuchumi au za kijamii kutokana na kutokuwa na utoshelevu wa mtaji.

### 1.2 MFUKO

Huu ni mfuko unaowahusisha wanachama wote wa NYUMBA SACCOS LTD ambao wanatimiza wajibu wao kwa kuchanga Akiba, kumiliki Hisa na kukopa mikopo kutoka kwenye Chama. Mfuko huu utazingatia kukinga majanga kwa mwanachama anaposhindwa kurejesha mkopo kwa sababu zilizo nje ya uwezo wake.

Mfuko huu ni tofauti na matengo ya lazima ambayo yapo kwa mujibu wa sheria ya ushirika. Mwanachama atakatwa asilimia moja (1%) katika kila mkopo atakao kopa.

### 1.3 MADHUMUNI YA MFUKO

Madhumuni makubwa kufidia hasara inayoweza kutokea kwa NYUMBA SACCOS LTD kwa mwanachama atakapokuwa amepatwa na ulemavu wa kudumu ambao utamfanya ashindwe kupata kipato. Aidha mfuko utatumika kutoa rambirambi kwa mwanachama atakayefariki au kufiwa na mwenza wake, baba mzazi au mama mzazi au mwanaye wa kuzaa [*Biological child*]. Ili mradi watoto hawa wasizidi idadi inayotambuliwa na Serikali.

Mtoto anayetambuliwa ni yule ambaye umri wake hauzidi miaka kumi na nane au umri wa miaka 21 kwa anayesoma.

### 1.4 UMILIKI WA MFUKO

Mfuko utamilikiwa na NYUMBA SACCOS LTD.

### 1.5 UCHANGIAJI WA MFUKO HUU

Mfuko utachangiwa na wanachama wote wanaokopa katika mikopo katika SACCOS kwa mikopo kukatwa asilimia 1% ya mkopo isipokuwa mikopo ya mwisho wa juma (week end), sikukuu na bima ya vyombo vya moto. Kiasi hiki kitawekwa katika akaunti maalum ya mfuko wa tahadhari ili kuwezesha dhamira hii kutekelezwa bila changamoto yoyote.

### 1.6 HIFADHI YA FEDHA ZA MFUKO

Fedha za mfuko zitafunguliwa akaunti maalumu katika benki na hazitatumika kwa kwa namna nyingine tofauti na madhumuni yaliyokusudiwa.

### 1.7 MAFAO YATOKANAYO NA MFUKO HUU

a) NYUMBA SACCOS LTD kupitia mfuko wa tahadhari, utasimamisha makato ya mkopo wa mwanachama aliyekatwa makato ya asilimia (1%) ya mkopo wake kama tahadhari endapo atafariki au kupata ulemavu wa kudumu uliothibitishwa na daktari kabla ya makato ya mkopo wake hayajamalizika, ulemavu wa kudumu ambao utasababishia kutokuwa na uwezo wa kupata kipato;

b) Endapo mwanachama wa NYUMBA SACCOS LTD atafariki, NYUMBA SACCOS LTD kupitia mfuko wa tahadhari itatoa, itamkabidhi mrithi wa marehemu kiasi cha Tzs. 500,000/= Kama rambirambi ya SACCOS kwa familia ya mwanachama (mrithi aliyeandikwa na mwanachama katika kitabu cha mwanachama);

c) Endapo mwanachama wa NYUMBA SACCOS LTD atafiwa na mwenza wake, NYUMBA SACCOS LTD kupitia mfuko wa tahadhari itatoa/itampa mwanachama aliyefiwa, kiasi cha Tsh. 500,000/= kama rambirambi;

d) Endapo mwanachama wa NYUMBA SACCOS LTD atafiwa na mtoto wake wa kumzaa [Biological child] NYUMBA SACCOS LTD kupitia mfuko wa tahadhari itatoa/ itampa mwanachama aliyefiwa na mtoto wake, kiasi cha Tsh. 500,000/=;

e) Endapo mwanachama wa NYUMBA SACCOS LTD atafiwa na wazazi wake chama kupitia mfuko wake wa tahadhari kitatoa kwa mwanachama rambirambi kiasi cha shilingi 500,000/=.

## 1.8 UTARATIBU WA KUWASILISHA MAOMBI PAMOJA NA NYARAKA ZA KUAMBATANISHA

a) Mwakilishi wa mwanachama au mwanachama mwenyewe, mwenzi wa mwanachama atatakiwa kutoa taarifa za kifo, au kufiwa na mke au mtoto ndani ya kipindi cha miezi mitatu toka kifo kilipotokea na taarifa hizo zitaletwa kwenye ofisi ya Chama kwa namna ambayo itakuwa imekubalika na Chama.

b) Nyaraka na vithibitisho vitakavyohitajika kama ushahidi ni kama vifuatavyo:-

1. Kwa mwanachama aliyefariki; -
    - i. Nakala ya cheti cha kifo/ hati ya mazishi au uthibitisho wa Afisa mtendaji kata au kijiji
    - ii. Salary slip ya mwezi aliofariki.
2. Kwa mwanachama aliyefiwa na mwenzi wake; -
    - i. Nakala ya cheti cha kifo au mazishi;
    - ii. Barua ya mtendaji wa serikali za mtaa inayothibitisha kwamba mhusika amefariki. (kwa mwanachama/ mwenza) aliyefia kijijini mahali ambapo hati ya kifo au cheti cha mazishi hakiwezi kupatikana na
    - iii. Nakala ya cheti cha ndoa iliyopitishwa na hakimu au mwanasheria.
3. Kwa mwanachama aliyefiwa na mtoto wake; -
    - i. Awe ni mtoto wake wa kumzaa (*Biological child*);
    - ii. Nakala ya cheti cha kuzaliwa iliyopitishwa na hakimu au mwanasheria na
    - iii. Nakala ya hati ya kifo au hati ya mazishi na kama amefia kijijini barua ya Afisa Mtendaji
4. Taarifa nyinginezo kama barua pepe kutoka kwa mwajiri au wasimamizi wa mikoani zitakubalika na

5. Mwanachama atakayetoa taarifa za uongo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake, kwa kurejesha kiasi alichopewa kama rambirambi ikiwa ni pamoja na kulipa adhabu ya asilimia hamsini (50%) ya rambirambi kwa kipindi kisichozidi mwezi mmoja tu.

## 1.9 MAJUKUMU YA BODI JUU YA MFUKO

i. Bodi itahakiki makusanyo ya fedha ya tahadhari ikilinganishwa na mikopo iliyotolewa kwa kipindi husika;
ii. Taarifa ya matumizi na mwenendo wa mfuko, itatolewa katika Mkutano Mkuu.

## 1.10 UHUISHAJI NA UIDHINISHAJI WA MWONGOZO WA MFUKO

### 1.10.1 Uhuishaji wa Mwongozo

Mwongozo huu utafanyiwa mapitio kila mwaka na unaweza kuhuishwa mara moja ndani ya mwaka ama kulingana na mahitaji na inapostahili.

### 1.10.2 Uidhinishwaji wa Mwongozo

Mwongozo huu wa Mfuko umeandaliwa na Bodi ya Chama na kupitishwa na wanachama kwenye Mkutano Mkuu wa………. uliofanyika tarehe..................... na itaanza kutumika baada ya kuidhinishwa na Mrajis.

| | |
|---|---|
| ……………………… | ………………… |
| **Mwenyekiti** | **Meneja** |